

# Mpango wa Msaada wa Chakula cha Dharura

Julai 2006

Mpango wa Msaada wa Chakula cha Dharura (TEFAP) hutoa chakula cha bure kwa kaya ambazo zina mapato ya chini. TEFAP husafirisha chakula yamkini mara nne au zaidi kwa mwaka kwa akiba za chakula na vyombo vya msaada. Ili kujifunza ni wapi na ni lini unapaswa kuchukua chakula, watu wanaweza kuwasiliana na akiba ya chakula iliyo mtaani, chombo cha msaada, au ofisi ya SRS. Ili kustahili, watu lazima wafanye yafwatayo:

- Watie saina karatasi, wakisema kwamba wanastahili TEFAP. Lazima watie saina karatasi kabla ya kuchukua chakula.
- Watoe kiwango cha mapato yao na ukubwa wa kaya.
- Watoe dhibitisho ya mapato na ukubwa wa kaya, ikiwa wataulizwa.
- Waishi Kansas.
- Waombe katika mkoa wao wa nyumbani.
- Fuata maombi mengine ya mtaani.

## VIWANGO VYA UPEO VYA MAPATO TASLIMU YA KILA MWEZI

<u>Ukubwa wa Kaya</u>	<u>Upeo wa Mapato</u>	<u>Ukubwa wa Kaya</u>	<u>Upeo wa Mapato</u>
1	\$1,062	5	\$2,535
2	\$1,430	6	\$2,904
3	\$1,799	7	\$3,272
4	\$2,167	8	\$3,640

Kwa kila mtu wa ziada wa familia ongeza \$369

Upeanaji wa chakula unaweza kutofautina na soko la shamba. Vyakula vinaweza kujumuisha:

Mboga za Mkebe	Maharagwe Mbichi, Nafaka, Viazi, Dengu, Viazi Vitamu
Maharagwe Yaliyokaushwa	Maharagwe Nyeupe, Maharagwe Nyeusi
Matunda ya Mkebe	Mapea, Mapichi, Plamu
Maji ya matunda	Maji ya machungwa, Maji ya Matufaha, Maji ya Mizabibu
Nyama/Proteni	Ngombe, Nguruwe, Samaki
Nafaka Baridi	Nafaka ya Mahindi, Nafaka ya Mchele, Nafaka ya Shayiri
Matunda yaliyokaushwa	Cheri, Zabibu kavu, Plamu kavu

Zingine	Siagi ya Njugu, Biskuti, Mchele, Tambi, Maziwa Kavu, Supu
---------	---

[Habari kuhusu Maeneo ya Kugawanya Chakula \(.pdf, 91KB\)](#)

[Habari kuhusu Eneo la Kusafirisha Chakula \(.pdf, 703KB\)](#)

[Tovuti ya USDA ya Mipango ya Ugawanyaji Chakula na karatasi za Kweli](#)

[Ramani ya Misaada ya Chakula](#)

Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu TEFAP angalia Mwongozo wa Kansas wa Kugawanya Vifaa (KCDM) [Mwongozo wa KCDM](#) mkondoni au kwa shirika linalohusika.

*Kulingana na Sheria za Serikali na Idara ya Marekani ya Sera za Ukulima, taasisi hii imekatazwa kutokana na kubagua kwa misingi ya jamii, rangi, asili ya kitaifa, jinsia, umri au ulemavu.*

*Ili kuwasilisha malalamiko ya ubaguzi, andikia USDA, Director, Office of Civil Rights, Room 326-W, Whitten Building, 1400 Independence Ave. SW, Washington D.C. 20250-9410, au piga simu (202) 720-5964 (sauti na TTD). USDA ni mwajiri na mtoa nafasi sawa.*

Kwa huduma zingine, au kupata Ofisi ya Jamii na Urudishaji au Eneo la Kufikia lililo karibu na wewe, tumia viungo vilivyo mwisho wa ukurasa huu.

Ukurasa Ulisasishwa: Juni 20, 2006